amfn e.V.

Ein Projekt
der Arbeitsgemeinschaft
Migrantinnen, Migranten
und Flüchtlinge
in Niedersachsen (amfn e. V.)

migranten
eltern
netzwerk

www.men-nds.de



# Habari kuhusu Mfumo Wa shule

## Katika lower saxony

## Watoto Wetu Maisha Yetu ya Badaye

- Chekechea
- Mfumo wa shule
- Shule ya msingi
- Shule ya sekondari
- Utambuzi wa digrii ambazo umekuja nazo
- Mpito kutoka shule hadi kazini

Kiswahili



## Wazazi wapendwa,

Mchakato wa ujumuishaji kwa wahamiaji na wakimbiyi wapya ni Changamoto kubwa kwa kuwa mambo mengi huonekana mapya na yenye kushangaza katika wakati wa kwanza.
Mustakabali wa watoto na maendeleo yao shuleni, ni wasiwasi mkubwa kwa wazazi wanaotakia maisha na maendeleo bora ya watoto wao baadaye.
Mfumo wa elimu nchini Ujerumani ni tofauti na nchi nyingine.
Msingi wa mfumo huu ni kuhusika kwa wazazi pamoja na kuwasaidia watoto wao.Ushirikiano mwema kati ya walimu na wazazi ni muhimu.
Ndio sabau wazazi wanahitaji taarifa sahihi kuhusu elimu na mifumo ya shule katika Saxony ya chini Ujerumani.
Katika kijitabu hiki,tunaeleza baadhi ya mambo muhimu tukifahamu kuwa si maswali yote tuliweza kujibu.
Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na ofisi husika kwa mfano:
Ofisi ya shule katika manispaa au kujielekeza shule moja kwa moja.

## Sisi ni wakina Nani?

Mtandao wa wazazi Saxony ya chini Ujerumani inalenga kuboresha fursa za watoto wenye asili ya uhamiaji kushiriki shule na kukuza ujuzi wao.
Tunawakilisha pia maslahi yao kwa wanasiasa, utawala na watowaji maamuzi katika ngazi za serekali.

## Habari kwa watoto wadogo kutoka mwaka 1 hadi myaka 6

| | |
|---|---|
| **Kuanzia umri Gani mtoto Anaanza kupewa Huduma mchana?** | **Huduma ya mchana huanzia mtoto wa mwaka 1 hadi myaka 3**<br>Ikiwa mtoto wako tayari ana umri wa mwaka mmoja, ana haki kisheria yakutunzwa katika kituo cha kulelea watoto mchana. |
| **Kwanini mtoto Wangu aende Chekechea?** | - Watoto hujifunza lugha ya kijerumani haraka.<br>- kiwa ni lazima, mtoto hupewa msaada maalum wa lugha.<br>- Watoto wanatiwa moyo na kutayarishwa kwa ajili ya shule.<br>Umri wa myaka 5 lazima mtoto aende shule ya chekechea. |
| **Haki yakupewa Nafasi shule Ya chekechea** | **Chekechea/kituo chakulelea watoto: umri wa myaka 3 hadi 6**<br>Watoto katika umri wa myaka 3 hadi 6, wana haki ya kisheria Ya kupewa nafasi katika shule ya chekechea. |
| **Napataje Nafasi?** | Unapotuma maombi kwajiji, mfano; (Ofisi ya ustawi wa vijana, tovuti ya mtandaoni).<br>Na katika shule ya chekechea moja kwa moja, Inapo patikana nafasi utaarifiwa kwa ujumbe wa maandishi.<br>Tuma maombi yako sehemu tofauti maana si kila mahali upatikana nafasi kwa urahisi. |
| **Unaitaji kuja Na nini unapo tuma maombi?** | Taarifa za kibinafsi (cheti cha usajili,cheti cha kuzaliwa) cheti cha kuzaliwa cha mtoto wako kinapashwa kutafsiriwa kwa lugha ya Kijerumani.<br>Uthibitisho kwamba mtoto wako amepokea chanjo ya surua. |
| **Hadi lini Mtoto wangu atahudumiwa?** | Mda unatofautiana kulingana na kituo na nafasi iliyopo.<br>Kwa kawaida, mda wa matunzo ni kuanzia Saa 8:00 asubuhi hadi 14:30 mchana.<br>Inabidi umlete mtoto hapo kwa wakati, Na mda wakumchukuwa uje umchukuwe peke yako. |
| **Mtoto wangu Atapewa chakula?** | Kuna nyakati maalum za kifungua kinywa (chai ya asubuhi) Na chakula cha mchana. Wapashwa kuomba taarifa kwamba Kituo utowa huduma ya kifunguwa kinywa (chai ya asubuhi), au kulipa ada. Chakula cha mchana, kinategemea muda ambao mtoto wako yuko chini ya uangalizi.<br>Maranyingi kituo hutowa huduma mbadala kwa wasio Kula nyama ya nguruwe. |

## Habari kwa wazazi wa watoto
## Katika shule ya msigi (miaka 6 hadi 10)

| | |
|---|---|
| **Elimu ya lazima** | Katika saxony ya chini, kuna elimu ya lazima ya miaka 12 kwa watoto wote kutoka miaka 6 hadi 18.<br>Uandikishaji wa shule kwa kawaida hufanyika baada ya likizo za kiangazi (summer) mnamo Agosti/Septemba kila mwaka. |
| **Watoto wako Wanaanza lini Shule?** | Watoto wote wanaofikisha miaka sita ifikapo Juni 30 ya mwaka, wanatakiwa kwenda shule. Wazazi ambao watoto wao wanafikisha miaka sita kati ya mwanzo wa Julai na mwisho wa Septemba, hawaandikishwi wala kuanza shule moja kwa moja. Familia huamuwa wenyewe ikiwa watoto wao wataahirisishwa au la.<br>Ni lazima wafanye uamuzi wao hadi kufikia tarehe 1 Mei.<br>Watoto wengine wote ambao bado hawajawa tayari kabisa, (kimwili, kiakili, au kijamii)wanaweza kwenda shule mwaka 1 baadaye. |
| **Kabla ya kuanza kuanza shule.** | Watoto wanapashwa kuwa wamehudhuria shule ya Chekechea angalau kutoka umri wa myaka mi 5.<br>Tunapendekeza kuhojiwa kwa U8 wanapokuwa na umri Wa miaka 3 ili kujua hali ya ukuaji wa mtoto.<br>Mtoto hupewa mtihani wakuzungumza chekechea.<br>Ikiwa mtoto atafeli mtihani, utaalikwa kwa maandishi ikiwa Kwamba mtoto wako ataitaji uchunguzi wakimatibabu. |
| **Kuanza shule** | Kabla ya kuanza darasa la kwanza, mtoto wako atapokea mwaliko kutoka shuleni. Ikiwa umbali kutoka nyumbani hadi shule ni mkubwa sana, mtoto wako atapata Tiketi ya basi.<br>Shule itatoa taarifa zaidi kuhusu (Vitabu, Kalamu, madaftari).<br>Familia zinazo hitaji msaada, zinaweza kutuma maombi ya ruzuku kupitia kifurushi cha elimu na ushiriki (BuT). |
| **Masomo** | Kisheria watoto huanza masomo yao saa 8:00 asubuhi hadi saa 1:00 jioni.Mtoto wako anatakiwa kwenda shule kwa wakati.Ikiwa mtoto wako hawezi kwenda shule, piga simu shuleni utowe taarifa.<br>Ikiwa mtoto wako hayupo shule kwa zaidi ya siku tatu, unahitaji kutoa sababu ilio andikwa au cheti cha matibabu.<br>Fahamu jinsi gani watoto hupokea alama za shule.<br>Watoto hupokea alama 1-6.<br>1 ni alama kwamba mtoto yuko vizuri saana. Watoto wako wanaweza kupewa masomo yakurekebisha lugha.<br>Uliza! |

| | |
|---|---|
| **Ushirki wa wazazi** | Shule, walimu na wazazi wanahitaji ushirikianoi. Kila darasa kutakuwa na uchaguzi wa wazazi ambao uchaguliwa ili kusimamia wazazi wengine. |
| **Maswali?** | Kama una maswali yoyote au unahitaji taarifa, omba fursa yakuongea na mwalimu wa darasa. |



## Shule za sekondari baada yakuhudhuria shule ya msingi

Baada ya darasa la 4 la shule ya msingi, mtoto huenda shule ya sekondari. Wazazi mnaamua ni shule gani ya sekondari ambayo mtoto wenu anapashwa kwenda. Ushauri na nasaha, walimu watajulisha wazazi aina gani ya shule inafaa kwa watoto wenu kuanzia darasa la 5.
Uwezo wa mtoto wako unapashwa kuendana na aina ya shule iliyochaguliwa. Hii inajumuisha alama za shule, maslahi ya mtoto na urafiki uliopo na watoto wengine.

1 - Hauptschule

2 - Realschule

3 - Gymnasium

4 - Gesamtschule (Oberschule, IGS)

| | |
|---|---|
| **Hauptschule** | Hauptschule, inashughulikia miaka ya shule kuanzia darasa la 5 Hadi darasa la 9 au la 10.<br>Hauptschule huwapa wanafunzi wake elimu ya msingi ya ujumla na muelekeo wa mtu binafsi wa taaluma.<br>Baada ya mwaka wa darasa la 9 wa shule, unaweza Ukahudhuria darasa la 10 na kupata cheti cha Realschule. |
| **Realschule** | Realschule inajumuisha miaka ya shule kuanzia darasa la 5 hadi darasa la 10. Inatoa elimu ya ujumla iliyo panuliwa na muelekeo wa ujumla wa taaluma.<br>Baada ya mwaka wa 9 wa shule, hupatikana cheti.<br>Cheti hicho kinaruhusu kuhudhuria shule za ufundi. |
| **Gymnasium** | Gymnasium inajumuisha miaka ya schule kuanzia darasa la 5 hadi la 13. Huwapa wanafunzi wake elimu ya jumla pana na ya kina. Huwawzesha wanafunzi wake kupata Sifa za jumla za kitaaluma.<br>Mwishoni mwa mwaka wa 10 wa shule, wanafunzi hupokea digrii kulingana na ufaulu wao.<br>Baada ya darasa la 12, wanaweza kuhudhuria chuo cha ufundi. Unaweza ukahudhuri darasa la 13 na kufanya upate diploma (Abitur). |
| **Gesamtschule** | Gesamtschule huwapa wanafunzi wake elimu ya msingi pana na ya kina. Na haiwadhinishi kuendelea na elimu Yao inayohusiana na taaluma au inayohusiana na masomo.<br>Kawaida na matawi ya shule ya Hauptschule na Realschule. |

| | |
|---|---|
| | Cheti cha Hauptschule na Realschule kinaweza kupatikana. Katika shule ya Gesamtschule wanafunzi huwa kutoka Darasa la 5 hadi darasa la 13 Mnara huu wa shule haupo Katika nchi nyingine nyingi.<br>Realschule na Abitur zinaweza kupatikana,kulingana na na utendaji wa mtoto. |
| **Ni ipi nzuri kwa Mtoto wangu?** | Uwezo wa mtoto wako unapaswa kuendana na aina ya shule uliyochagua ikijumuisha alama za shule na mapendeleo ya mtoto.<br>Matukio ya habari na tovuti za shule husika, zaelekeza wazazi kwenye maamuzi sahihi. |
| **Maoni kwa wazazi** | Habari, mazungumzo, mikutano maswali au mazungumzo binafsi omba nafasi yakuonana na mwalimu anaye wajibika au mwalimu wa darasa. |



Baada ya mafanikio ya shule kukamilika, hatua inayofuata ni ya mafunzo ya ufundi(kazi) au chuo.

Si rahisi sana kupata kazi nchini ujerumani Hasa kwa wale ambao hawana elimu.

Mafunzo ya ufundi yanatokana na utendaji kazi.

Baada ya kuhitimu juhudi na uwezo wa kijana.

Mafunzo ya ufundi yana hadhi maalum nchini Ujerumani na ndio kadi ya wito kwa taaluma.

## Elimu ya mafunzo ya uwili

Mafunzo ya uwili ndio mfumo unaojulikana zaidi wa mafunzo ya ufundi nchini Ujerumani (Dual).
Ina maana kwamba sehemu ya mafunzo hufanyika katika kampuni (k.m. siku 4 kwa wiki). Na kushiriki katika shule ya ufundi (siku 1 kwa wiki). Hii inawezesha uhusiano kati ya nadaharia na vitendo. Takriban 2/3 ya wafanyakazi nchini ujerumani, wamefunzwa elimu hiyo.

### Muda na mwendo wa mafunzo

Mafunzo kwa kawaida huchukuwa myaka 2 hadi mi 3.
Katika shule ya ufundi, masomo yanayohusiana na taaluma maalum na ujuzi wa jumla hufundishwa (Kijerumani, siasa, michezo).

### Uteuzi

Mafunzo, ajira na ushauri, Wakala wa ajira unashauri na kusaidia vijana.

### Nafasi za uanafunzi

Kisheria maombi hufanyika katika kampuni.
Mshahara wa kila mwezi hutofautiana kutokana na kazi.
Mshahara ni kati ya Euro 400 na 600 na huongezeka baada ya kila mwaka.

Ujuzi wa lugha muhimu angalao kiwango B1.
Mkataba unahitimishwa na kampuni ya mafunzo.
Usajili katika shule ya ufundi ni bora.

| | |
|---|---|
| **Usajili wa shule** | Mbali na mafunzo katika mfumo wa pande mbili,fani zingine zinaweza pia kujifunza katika shule ya ufundi.<br>Masomo ni ya mda wote katika shule za ufundi za serekali, na mafunzo hayana malipo.<br>Shule za kibinafsi mafunzo hutozwa ada. |
| **Chuo kikuu** | Sifa la kusomea chuo kikuu kwa kawaida ni Abitur (sifa ya jumla ya kuingia katika elimu ya juu). Au sifa yakuingia katika chuo cha ufund ili ili kusoma katika chuo cha ufundi.<br>Kozi hiyo ni ya bure na inatambulika duniai kote kwa ubora wake.<br>Watu walio na hadhi ya ukimbizi pia wanaweza kwenda chuo, na pia kupata usaidizi wa kifedha chini ya sheria ya usaidizi wa (BAFöG). |
| **Nini wapashwa kuzingatia?** | Tafadhali tafuta ushauri kabla yakuchaguwa kazi.<br>Taasisi mbalimbali zinapatikana kwa madhumuni haya (k.m. kizuo cha taarifa za kazi BIZ katika wakala wa ajira, au huduma ya ushauri kwa wanafunzi ). |



# Utambuzi wa digrii za shule za kigeni

Watoto wengi wa shule wanao kuja Ujerumani wamehudhuria shule katika nchi zao. Kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule baada yakutambuliwa digrii za shule swali linakuja katika kujuwa ni shule gani au darasa la ngapi watapangiwa.
Katika Saxony ya chini kwa ujumla shule ndio inayo husika kupanga arasa ambalo wanafunzi wapya watakubaliwa.
Uamuzi wa shule unatokana na idadi ya myaka ya mahudhurio ya shule na idadi ya masomo yanayofundishwa katika nchi ya asili.


Vitu muhimu vinavyo itajika unapo kwenda kuomba shule:


- Kitambulisho au paspoti
- Kibali cha ukaazi
- Hati ya usajili kutoka manispaa
- Digrii zote za shule
- digrii zote zitafsiriwe kwa Kijerumani na (mtafisiri)
- Nakala za hati zote zilizotajwa

Ikiwa huwezi kutoa hati yoyote, tafadhali wasiliana na shule husika.
Ikiwa mtoto wako bado hajui lugha yakijerumani, mtoto wako atatiwa moyo ipasavyo na shule pia itakupa habari juu ya hili.



# Mfumo wa shule






# MAWASILIANO:


## MigrantenElternNetzwerk Niedersachsen

Kurt-Schumacher-Straße 29, 30159 Hannover

Tel.: (0511) 9215106 | Fax: (0511) 9215527

elternnetzwerk@amfn.de | www.men-nds.de



MigrantenElternNetzwerk Niedersachsen ya chini Ujerumani unafadhiliwa na:

Niedersächsisches Ministerium für Soziales, Arbeit, Gesundheit und Gleichstellung

MigrantenElternNetzwerk Niedersachsen ya chini unasaidiwa na:

Niedersächsisches Kultusministerium